HOTUBA YA MGENI RASMI, KATIBU MKUU WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA, DKT. LEONARD AKWILAPO KATIKA MAHAFALI YA ISHIRINI NA TANO (25) YA ADEM KWA WAHITMU WA STASHAHADA ZA UONGOZI NA USIMAMIZI WA ELIMU (DEMA) NA UKAGUZI WA SHULE (DSI) YANAYOFANYIKA CHUONI ADEM-BAGAMOYO SIKU YA IJUMAA TAREHE 24 NOVEMBA, 2017

Ndugu Mkuu wa Wilaya,
Ndugu Mtendaji Mkuu wa ADEM,
Ndugu Wahitimu,
Ndugu Wakufunzi na Wafanyakazi wa ADEM,
Ndugu Wanachuo wa ADEM,
Ndugu Wanahabari,
Ndugu Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

Ndugu Mtendaji Mkuu,
Napenda kutumia fursa hii kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai hadi leo hii tunapokutana katika mahafali haya ya Ishirini na tano (25) ya Kozi za muda mrefu zinazoendeshwa na ADEM.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako Mtendaji Mkuu wa ADEM kwa kunishirikisha na kunipa heshima ya pekee ya kuwa Mgeni Rasmi katika mahafali haya ya Ishirini na Tano (25) kwa wahitimu wa mafunzo ya Stashahada mwaka huu wa 2017. Pia, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wale wote waliowezesha kwa njia moja ama nyingine kufanikisha mafunzo haya, hususan kwa wakufunzi na wafanyakazi wa ADEM. Napenda pia kutambua mchango wa Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kuwapa ruhusa za kuja kusoma ADEM na baadhi yao kuwalipia ada walimu wanaohitimu leo hii na hata wale wanaoendelea na masomo kwa kampasi zote tatu Bagamoyo, Mbeya na Mwanza.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Kuja kwangu hapa Bagamoyo kumenipa nafasi ya kujionea mwenyewe shughuli zinazofanywa na ADEM katika kuboresha mazingira ya utoaji mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu pamoja na Uthibiti Ubora wa Shule. Miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na kuendesha mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa njia ya masafa katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe chini ya ufadhili wa UNICEF. Fursa hii pia imenipa nafasi muhimu ya kukutana na kuongea na wahitimu ambao wamepikwa vya kutosha katika nyanja za Uongozi na Usimamizi

wa Elimu na Uthibiti Ubora wa Shule kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi katika shule za msingi nchini.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Nimeambiwa kwamba haya ni mahafali ya Ishirini na Tano (25) ya wanachuo wanaohitimu mafunzo ya Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu ambao wapo **417** na Stashahada ya Ukaguzi wa Shule wapo **319** wanaohitimu leo. Hii inafanya jumla ya wahitimu wote kuwa **736**. Ninaelewa wazi kwamba mafunzo yatolewayo na ADEM yanalenga kuongeza uwezo wa kiutendaji kwenye taasisi za elimu pamoja na kukabiliana na changamoto zilizopo katika sekta ya Elimu kwa ujumla, na hivyo kuboresha uendeshaji wa elimu na kuwawezesha wanafunzi kupata Elimu bora. Lengo ni kwenda sambamba na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ambapo Tanzania imeanza kutekeleza ujenzi wa Uchumi wa kati kupitia viwanda, Mkakati wa Kitaifa wa Kupunguza Umaskini na Kukuza Uchumi (MKUKUKTA) na Sera ya Kimataifa ya Elimu kwa Wote (EFA) ambazo zote zinatambua umuhimu wa elimu bora katika kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Naamini kuwa wanachuo mliohitimu mafunzo ya Stashahada za DEMA na DSI mtakuwa mmepata maarifa, mbinu sahihi na stadi ambazo zitawawezesha kutekeleza majukumu yenu.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Ni matarajio ya Serikali kuwa Wahitimu wa Kozi za Uongozi na Usimamizi wa Elimu mara mrudipo shuleni mtaweza kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (2014), Sheria, Kanuni na Taratibu za Elimu ili kupunguza migogoro shuleni na kudhibiti nidhamu za wanafunzi. Wahitimu pia mnapaswa kusimamia utekelezaji wa Mtaala kwa ufanisi mkubwa, kutoa takwimu sahihi za shule, kupanga mipango ya maendeleo ya shule inayotekelezeka, kusimamia fedha za elimu bila malipo pamoja na rasilimali zingine za shule, kusimamia ustawi wa walimu na wanafunzi, kushirikisha jamii na wadau wa Elimu katika shughuli za maendeleo ya shule pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli zinazotekelezwa shuleni.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Serikali pia inamatarajio makubwa kwa wahitimu wa kozi ya Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Shule kwamba mtaweza kusaidia kuthibiti ubora wa shule kwa kusimamia Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) Sheria, Kanuni na Taratibu za Elimu, kuanzisha Timu za Ukaguzi za ndani ya shule kabla wakaguzi kutoka nje hawajafika, kufanya tafiti ndogo zinazohusu changamoto zinazozikabili shule kama vile utoro uliokithiri, mimba za utotoni na nidhamu mbaya kwa baadhi ya wanafunzi shuleni. Wahitimu pia mnapaswa kutoa ushauri kwa uongozi wa shule

kuhusiana na utekelezaji wa mtaala, utunzaji rasilimali za shule, utoaji wa takwimu sahihi za shule, kudhibiti majanga shuleni, kupima maendeleo ya wanafunzi kwa njia ya majaribio na mitihani, kuratibu Malezi ya Kitaaluma na Kitaalamu kwa walimu wapya (Teacher mentoring) na kutoa ushauri na unasihi kwa walimu na wanafunzi.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu pamoja na Ukaguzi wa Shule katika nchi yetu ni muhimu katika kuwapa uwezo walimu na viongozi wa elimu kufanya kazi zao kwa weledi, ufanisi na kwa kujiamini zaidi hususani katika kipindi hiki cha maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia. Wahitimu kwa mantiki hiyo mnapaswa kuwa chachu ya mabadiliko katika Uongozi na Utawala Bora pamoja Uthibiti Ubora wa Shule nchini kwa kutumia ujuzi, maarifa, stadi na mbinu mpya mlizozipata katika mafunzo yenu ya miaka miwili. Aidha, maarifa mliyoyapata mkayaeneze kwa walimu ambao hawajapata fursa ya kupata mafunzo haya ADEM.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Ni matarajio ya serikali na taasisi mbalimbali za kielimu nchini kuwa zitawatumia vyema mahali popote pale watakapokwenda kufanya kazi kwa kutumia maarifa na ujuzi walioupata hapa

ADEM. Nawataka mkaoneshe kwa vitendo elimu mliyoipata katika kutumikia nafasi mbalimbali mtakazopangiwa na waajiri wenu. Nashawishika kusema kwamba ninyi ndiyo mabalozi na kioo cha chuo hiki katika kutoa mfano wa uongozi na utawala bora, uchapaji kazi, uzalendo pamoja na uadilifu katika kulitumikia Taifa letu.

Kwa upande wetu Serikali tutajitahidi kuwapa kipaumbele Wahitimu kutoka ADEM katika uteuzi wa Viongozi na Wathibiti Ubora wa Shule ngazi ya Shule, Kata na Halmashauri. Changamoto kubwa ni vigezo vya uteuzi ambavyo vinaenda sanjari na viwango vya Elimu. Hivyo, nawasihi msibweteke na mafanikio haya. Endeleeni kusoma zaidi hadi ngazi ya Shahada ya kwanza, Uzamili (Masters) na Uzamivu (Ph.D).

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Uongozi na Usimamizi bora wa elimu pamoja na Uthibiti Ubora wa Shule ni muhimu sana kwa sababu viongozi wa elimu wanatazamiwa kufanya kazi zao kwa utaalamu na ujuzi wa hali ya juu ambao huleta tija kazini na kuleta matokeo ya haraka yanayopimika kwa kutumia nyenzo za kisasa zinazotokana na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia. Tunawaomba wahitimu muwe ni chachu ya mabadiliko ya uongozi wa elimu pamoja na uthibiti ubora wa shule nchini kwa kutumia ujuzi, maarifa,

mwelekeo na mbinu mpya mlizozipata katika kuongeza ufaulu wa wanafunzi katika mitihani.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Serikali inatambua na kuthamini kazi za kitaaluma na kitaalam zinazofanywa na ADEM chini ya Uongozi wa Dkt. Siston Masanja Mgullah. Nimeambiwa kwamba kwa mwaka jana 2016 ADEM iliendesha na kusimamia mafunzo kwa walimu wa darasa la III na IV katika kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Jumla yua walimu **31,993** walipata mafunzo. Hongereni sana.

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kuisapoti ADEM katika kuboresha mazingira ya utoaji mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kufikia malengo ya kuandaa viongozi na wathibiti ubora wa shule wenye weledi stahiki.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kuongeza wigo wa kupata elimu bora nchini. Hatua kadhaa zimeshachukuliwa na utekelezaji wake unaonekana. Baadhi ya hatua hizo ni kujenga mazingira rafiki ya kutoa Elimu bila malipo kwa lengo la kuongeza fursa ya watoto

wengi kupata ElimuMsingi. Mitaala nayo imeboreshwa kwa lengo la kujenga umahiri unaotakiwa katika kila ngazi ya Elimu. Maboresho ya mtaala yameenda sambasamba na utoaji Mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu namna ya kuchambua Sera ya Elimuna Mafunzo (2014), kuwezesha walimu kufundisha kwa ufanisi Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK), kuchambua mtaala mpya (2016) na vipengele vyake, kuandaa masomo, kupima maendeleo ya kitaaluma ya mtoto na kuweka kumbukumbu za wanafunzi kwa usahihi. Aidha masomo ya sayansi yametiliwa mkazo kwamba kila mwanafunzi katika ngazi ya ElimuMsingi lazima asome masomo ya Sayansi ikiwa ni maandalizi ya kuandaa Rasilimali watu watakaotumika kuleta mageuzi ya Maendeleo nchini.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Serikali pia inaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kukarabati shule kongwe za sekondari na vyuo vya Ualimu. Lengo la Serikali ni kukarabati shule na vyuo vyote vikongwe kutegemea na upatikanaji wa fedha ili viweze kutoa Elimu bora.

Serikali pia inaendelea kuboresha utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini kulingana na uhitaji na uwezo wa fedha serikalini. Lengo ni kutoa mikopo kwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaochaguliwa kusoma vyuo vikuu nchini.

Mafunzo ya Ualimu nayo yameboreshwa ambapo mitaala yote inaandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania na kutahiniwa na Baraza la Mitihani la Taifa kwa mjibu wa Sheria. Tayari hatua zimeshachukuliwa na utekelezaji unaendelea.

Sanjari na hilo, Serikali imendelea kutoa Elimu bila malipo katika ngazi ya ElimuMsingi kwa kutoa ruzuku ya uendeshaji kwa shule za msingi na sekondari nchini. Hatua zote hizi zinalenga kuimarisha utoaji wa Elimu nchini ikiwa ndio nyenzo ya kufikia uchumi wa kati.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Nitumie fursa hii kwa niaba ya Serkali kuwataka Wahitimu wote kuitumia vizuri elimu mlioyoipata hapa ADEM katika kutekeleza wajibu wenu na katika kupambana na changamoto zinazojitokeza katika mchakato mzima wa utoaji Elimu nchini. Aidha, nawaelekeza mkatumie maarifa mliyopata kwa kushirikiana na walimu wengine hususani Walimu Wakuu katika kutoa takwimu sahihi za wanafunzi na mahitaji ya shule. Kumejitokeza tatizo kwa baadhi ya Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule kutoa takwimu zisizo sahihi ili kujipatia ruzuku kubwa. Takwimu zisizosahihi zinazotolewa ngazi ya shule zinasababisha Serikali kushindwa kujua mahitaji halisi yatakayofanikisha kupanga mipango ya maendeleo inayotekelezeka.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Masuala mengine ambayo pia ni muhimu kuyazingatia ni utunzaji wa mazingira, kupiga vita rushwa, mapambano dhidi ya madawa ya kulevya na kuzia maambukizi ya virusi ya ugonjwa wa UKIMWI. Masuala haya ni mtambuka hivyo yana athari mbaya kwa mtu binafsi, taasisi na taifa kwa ujumla. Uharibifu wa mazingira husababisha mabadiliko ya tabianchi na matokeo yake ni ukame, mafuriko na majanga mengine. Nchi ikikumbwa na ukame kutakuwa na tatizo la maji, njaa, na mlipuko wa magonjwa. Hali ambayo itasababisha wanafunzi, wazazi, walimu na wasimamizi wa elimu kutotekeleza majukumu yao ipasavyo. Aidha, rushwa inawanyima watu haki ya kupata huduma stahiki hususani wenye vipato vidogo, wanawake na watoto. Na katika sekta ya elimu, rushwa inaathari mbaya zaidi kwa sababu huwanyima watu wenye sifa nafasi za masomo, ajira na hata kupandishwa vyeo. Madawa ya kulevya pamoja na maambuki ya virusi ya UKIMWI yanaathari mbaya katika afya za walimu wetu, wanafunzi na wananchi wote kwa ujumla. Shule na taasisi zote za Elimu zinapaswa ziwe na watu wenye afya njema wenye uwezo wa kutimiza malengo yaliyowekwa.

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Kwa kuhitimisha, napenda kuwakumbusha wahitimu kuwa mafunzo muliyopata yasiwe ya mwisho bali yawe ni chachu ya kujiendeleza zaidi kitaaluma hususani katika nyanja hizi za Uongozi na Usimamizi wa Elimu pamoja na Uthibiti Ubora wa Shule hadi mfikie hatua ya juu zaidi. Vilevile kumbukeni maneno ya wahenga *“Elimu haina mwisho”*, hivyo mkiwa kazini muendelee kujifunza kupitia mifumo rasmi na isiyo rasmi ili kujiimarisha zaidi Kitaaluma na Kitaalam. Itapendeza sana!

Ndugu Mtendaji Mkuu,

Baada ya kusema hayo, napenda kutumia fursa hii kuwatakia baraka tele na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa kazi zenu za kila siku katika shule zenu. Mwisho nawatakia safari njema ya kurudi sehemu mbalimbali za kazi mkiwa na sura mpya ya utendaji kazi ili kuleta mbadiliko yenye tija katika sekta ya elimu nchini.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA